

SOKO LA USIKU LA MWANGA (KIGOMA)

Mradi wa kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji (LIC) ni mradi wa kuendeleza sekta binafsi unaofadhiliwa na Danida. Mradi unashughulikia vikwazo vikuu vinavyokwamisha maendeleo ya biashara na ukuaji wa uchumi katika ngazi ya wilaya kwenye mikoa miwili ya Dodoma na Kigoma nchini Tanzania. LIC imejikita katika mijadala kati ya sekta ya umma na sekta binafsi, miundombinu ya utoaji wa huduma za biashara ikiwa ni pamoja na vituo vya pamoja vya biashara na miundombinu ya pamoja kati ya sekta ya umma na sekta binafsi ili kusaidia maendeleo ya biashara na uwekezaji. Washirika wanaotekeleza mradi wa LIC ni Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Sekretariati za mikoa ya Kigoma na Dodoma, Baraza la Taifa la Biashara (TNBC) Tanzania, Jumuiya ya Tawala za Mitaa Tanzania (ALAT), Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), Chemba ya Wafanyabiashara, Wenye Viwanda na Kilimo Tanzania (TCCIA).

Mnamo mwezi wa saba mwaka 2017, LIC ilikubali ombi la Manispaa ya Kigoma Ujiji kusaidia ujenzi wa soko la usiku la Mwangi. Biashara ya usiku hapo nyuma ilikuwa inafanyika kandokando ya barabara kuu kuelekea Kigoma mjini ambapo ilikuwa hatari kwa ajali za barabarani kwa watu na wafanyabiashara. Hakukuwa na vifaa /mazingira safi wala huduma ya chuo iliyokuwa inatolewa japo bidhaa za chakula kama vile samaki zilikuwa zikiuzwa na kununuliwa kwa kiasi kikubwa. Kusudi la kujenga soko la usiku ilikuwa kutengeneza soko salama lenye taa na vyoo ambavyo vitasaidia wafanyabiashara wadogo - wengi wao wakiwa ni wanawake kufanya biashara kwenye mazingira safi na salama.



Soko la usiku la Mwangi, kwa ufadhili wa LIC. Kigoma Ujiji

Mambo muhimu ya mradi na mafanikio

Soko limejengwa na limeanza kufanya kazi tangu tarehe 20 ya mwezi Novemba, mwaka 2018 na limekuwa msaada mkubwa kwa wafanyabiashara na wateja. Barabara ya pembeni kutoka barabara kuu imechongwa na taa za umeme wa jua zimewekwa kadhalika vyoo na mfumo wa maji taka. Soko kwa kawaida linafanyika kuanzia saa 10:30 jioni mpaka saa 4 usiku na linahudumia wateja wote wanaoshindwa kupata mahitaji yao ya majumbani kwa muda wa asubuhi na mchana, lakini pia kwa wafanyabiashara wadogo wanao nunua bidhaa kwajili ya kuuza siku inayofatia.

Tayari mpaka sasa kuna uhitaji wa eneo la ziada na uwekezaji katika eneo linalozunguka soko kama vile sehemu za kula, maduka yanaendelea kufunguliwa, vyote vikiongeza mabadiliko chanya katika eneo linalozunguka soko.

Uwekezaji kwa awamu ya pili utaendeleza ujenzi kwa kuweka vigae kwenye eneo la soko lililobakia kwaajili ya wafanyabiashara. Aidha usafi unaohusiana na biashara ya samaki wabichi utaimarishwa kwa kuweka mifumo ya usambazaji maji na mfumo wa kutolea uchafu unaotokana na kusafisha na kukatakata samaki. Soko likikamilika litakuwa na uwezo wa kuchukua wafanyabiashara wadogo 450 na kwa kiasi kikubwa hili litapunguza tatizo la maeneo yasiyo rasmi kutumika kwa biashara na kuimarisha mazingira ya biashara ya Kigoma mjini.



Soko la usiku la Mwanga, kwa ufadhili wa LIC. Kigoma Ujiji

Zaidi ya kutengeneza mazingira bora kwa wafanyabiashara na wateja, soko jipya limetengeneza fursa za ajira za moja kwa moja kwa watoa huduma kwenye eneo la usafi na kazi zingine saidizi.

Kupitia ufadhili unaofanywa na mradi wa LIC, KUMC kwa kutumia rasilimali zake imeweza kuweka mazingira ya biashara yanayovutia ambayo pia yamekuwa chanzo kikubwa cha mapato kwa halmashauri.

LIC imewekeza kiasi cha shilingi milioni 95 katika kujenga soko la usiku la Mwanga, mradi pia unaendelea kusaidia miradi ya maendeleo ya sekta binafsi katika mikoa ya Dodoma na Kigoma.

Kwa taarifa zaidi, tafadhali tembelea tovuti ya mradi wa LIC: www.lic.or.tz

Disemba 2018